



26/04/2018

TAARIFA KWA UMMA JUU YA 'KIDUDU MTU'

Kama mnavyofahamu, kumetokea taharuki kwa wananchi kutokana na madai ya kuonekana kwa mdudu anayefahamika kwa jina la '*kidudu mtu*'. Kutokana na hali hiyo, wananchi wameacha kula mbogamboga na baadhi ya matunda kwa hofu ya kupoteza maisha.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji inawatangazia kama ifuatavyo:

- Hakuna ushahidi wowote wa kitaalamu wa kuhusisha mdudu huyu na afya za walaji wa mazao ya kilimo-yakiwemo mbogamboga na matunda. Hivyo, wananchi waendeleo na ulaji wa vyakula hivyo bila hofu yoyote.
- Wananchi wote wanakumbushwa kuzingatia utaratibu wa kawaida wa usafi wa vyakula kuanzia maandalizi kabla ya kupika na wakati wa kupika. Mkazo juu ya usafi uwekwe katika vyakula vinavyopikwa kwa muda mfupi kama vile mbogamboga na ambavyo havipikwi kabisa kama vile matunda.
- Mnakumbushwa kuwa si mara ya kwanza kwa mdudu huyu kuonekana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Hata hivyo, mtu yeyote anayehisi ameathiriwa na mdudu huyu kwa kula mbogamboga na matunda ajitokeze kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu.

Imetolewa na:

Thomas M. Shilabu

Kny Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya-Meatu